Barry, A. L., WHAT ABOUT? HOLY BAPTISM
- *Swahili*

Kuhusu Jambo Gani...

# Ubatizo Mtakatifu

**Daktari A. L. Barry**
**Rais**
**Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri**

Iwapo kungekuwa na daktari, kwa wakati, ambaye angekuwa na kipawa cha ajabu kiasi kwamba, angeweza kuwazuia watu wasife, na kuwafufua wale waliokwisha kufa, ili wasife tena. Fikiria tu, ni watu wangapi ambao wangefanya linalowezekana ili waweze kuponywa na daktari huyu! Sasa fikiria kwamba, katika Ubatizo Mtakatifu, hakika Mungu hutupatia kipawa cha uzima wa milele! Hebu tujifunze zaidi juu ya baraka hizi za ajabu.

**Ubatizo ni Nini?**

Ubatizo si maji matupu, bali ni maji yanayotumika kulingana na amri ya Mungu na kuchangamana na Neno la Mungu.

Je, maji haya ya kawaida machache yana umuhimu gani? Hayana chochote, mpaka Mungu alichangamanishe Neno Lake nayo! Katika Ubatizo, hilo ndilo alitendalo Mungu. Analichangamanisha Neno Lake liletalo uhai na lihuishalo na maji ya Ubatizo Mtakatifu, na kwa sababu hiyo, tunazaliwa upya kwa maji na kwa Roho (Yohana 3:5).

**Neno Hilo la Mungu ni Lipi?**

Katika sura ya mwisho ya Mathayo, Kristo Bwanawetu husema: "Basi enendeni mkayafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu." [Mathayo 28:19].

Bwana wetu huuamuru Ubatizo. Si wa hiari, wala siyo tu "ziada nzuri." Neno la Mungu huchukua sura nyingi, kufuatana na mapenzi Yake mema na yenye rehema. Neno Linahubiriwa, linafundishwa, na kutangazwa. Linasomwa, linachunguzwa, na kutafakarika. Wakristo, wasiokuwa Wakristo na waumini wenzao wanalishiriki kwa namna ile ile. Na ni Neno hilo la Mungu, ahadi Yake, inayoufanya Ubatizo kuwa ulivyo.

Mungu mwenyewe huwepo jina Lake linapochangamanika na maji, pamoja na uwezo Wake wote na baraka Zake zote za msamaha, uzima na wokovu. Kristo huyabariki maji ya Ubatizo kwa Neno Lake, hivyo, tunaposimama katika Ubatizo pamoja na Kristo majini, Baba hutuita wanawe wapendwa, tunapewa Roho Mtakatifu, na mbinguni inafunguliwa kwetu.

Wale wanaopata Ubatizo baada ya kuletwa katika imani kwa mahubiri au mafundisho ya Neno vile vile hupokea baraka zote ambazo Mungu amezichangamanisha na Ubatizo.

**Je, Ubatizo Huzitoa Faida gani?**

Huutoa msamaha wa dhambi, na huokoa kutoka mautini, kutoka kwa Ibilisi, na huutoa wokovu wa milele kwa wote wanaouamini, kama maneno na ahadi za Mungu vinavyotangaza. Maneno haya na ahadi hizi za Mungu ni zipi? Katika sura ya mwisho wa Marko, Bwana wetu Yesu Kristo husema : "Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa" [Marko 16:16].

Katika na kwa njia ya Ubatizo, Mungu hutusafisha dhambi zetu zote, hutunyakua kutoka kwa nguvu ya Shetani, na hutupatia uzima wa milele. Yote ni kazi ya Mungu anapotupatia baraka Zake. Ni ahadi Yake. Katika Ubatizo, Mungu wetu wa Utatu humgawia kila mmoja wetu binafsi vipawa ambavyo Bwana Yesu Kristo aliushindia ulimwengu kwa njia ya uhai, mateso, mauti, na kufufuka Kwake. Tafadhali soma hasa Gal. 3 :27 ; Kol. 1 :13-14 ; 1 Petro 3 : 21 ; Tito 3 :5-7 na 1 Kor. 6 :11.

**Maji Yanawezaje Kuyatenda Matendo Haya Makubwa?**

Hakika, si maji yatendayo matendo haya, bali Neno la Mungu linalochangamana na maji, pamoja na imani inayoliamini Neno hili la Mungu katika maji. Kwa kuwa pasipo Neno la Mungu, maji ni maji matupu na si Ubatizo. Lakini yanapochangamana na Neno la Mungu huwa Ubatizo, yaani, maji yahuishayo, yajaayo neema na kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili katika Roho Mtakatifu, Mtume Paulo asemavyo katika Tito sura ya tatu: "Alituokoa kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya katika Roho Mtakatifu, ambaye

alitumwagia kwa wingi, kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; ili tukihesabiwa haki kwa neema [Y]ake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele kama lilivyo tumaini letu. Ni neno la kuaminiwa" [Tito 3:5b-8a].

Naam, maji ya kawaida hayawezi kutenda matendo makubwa kama hayo, lakini maji ya Ubatizo si maji ya kawaida! Ubatizo ni njia moja ya pekee ambayo kwa hiyo Mungu hutupatia baraka alizotushindia Kristo. Ubatizo si kazi tuitendayo, bali ni kazi aitendayo Mungu. Kwa hiyo, ni zaidi ya ishara. Ni tendo takatifu ambalo kwa hilo Mungu Mwenyewe huwa kazini akisamehe dhambi, akitoa uhai mpya katika Kristo na akimtoa Roho Mtakatifu pamoja na vipawa Vyake vyote. Ubatizo hutupatia imani ambayo kwayo tunapokea vipawa hivi. Mungu, Roho Mtakatifu hufanyiza imani katika ahadi zinazochangamana na Ubatizo.

### Kubatizwa Huku kwa Maji kuna Maana Gani?

Kunaashiria kwamba, inapasa Adamu wa Kale aliye ndani yetu, kwa majuto makubwa na toba, kuzamishwa hadi kufa pamoja na dhambi zote na tamaa mbovu, na kwamba, inapasa mtu mpya kuibuka na kuinuka kila siku na kuishi milele mbele za Mungu katika haki na usafi. Haya yameandikwa wapi? Katika Warumi sura ya sita, Mt. Paulo huandika: "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya [U]batizo katika mauti [Y]ake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima" [Warumi 6:4].

Katika Ubatizo, tunazikwa pamoja na Kristo, na katika Ubatizo tunafufuliwa pamoja na Kristo. Mauti Yake na kufufuka Kwake vinafanywa kuwa vyetu wenyewe, na kwa sababu ya ukweli huo, katika uhai wetu wote, tunaweza kusema, "Nimebatizwa!" Kwa kuwa tulizikwa pamoja na Kristo katika mauti Yake, hatupaswi kuliogopa kaburi ambamo siku moja tutazikwa. Kristo amekwisha kuwa humo tayari. Katika Ubatizo Mtakatifu, tunalipitia kaburi Lake na kufikia kufufuka Kwake.

Asemavyo Luther katika Katekisimo Kubwa yake, "Ikiwa nimebatizwa, nina ahadi kwamba, nitaokolewa na kuwa na uzima wa milele, katika roho na katika mwili . . . hakuna johari kubwa iwezayo kuipamba miili yetu na roho zetu kuliko Ubatizo . . . Ubatizo ni hazina ambayo Mungu hutupatia na imani hushikamana, ambavyo si kazi ya binadamu kwa Bwana Kristo kuwa msalabani, bali ni hazina inayofahamika na kutolewa kwetu katika Neno na kupokewa kwa imani."

### Je, Ubatizo Una Nini kuhusu Maisha Yetu ya Kila Siku?

[Ubatizo] una kila kitu! Maisha yetu yote ni maisha tuanayoishi tukizitegemea ahadi za Mungu, zilizotolewa kwetu katika na kwa njia ya Ubatizo Mtakatifu. Tunarudia Ubatizo siku zote. Nyakati za majaribu na mateso katika maisha yetu, wakati yote yanaonekana kutulemea kabisa, na hasa nyakati zile ambazo dhambi yetu na hatia ya dhambi hizo huturudia mara kwa mara, tunaweza, asemavyo Luther, "Kuutoa Ubatizo wetu na kuutikisa chini ya pua ya ibilisi na kusema, 'Nimebatizwa . . . nimeoshwa na Mungu. Ni damu ya Kristo mwenyewe.' Ni kuoshwa kulikobarikiwa na kuchanganywa na damu ya Kristo." Hatuwezi kuurudia msalaba wa Kristo, wala hatuwezi kuwaza wenyewe kuwa huko tena. La, badala yake tunaugeukia ukweli wa kazi ya Mungu "wakati huu" katika maisha yetu. Tunaurudia Ubatizo wetu. Maana ilikuwa ni papo hapo ambapo Mungu alituzika pamoja na Kristo na kutufufua pamoja Naye ili tuwe na maisha mapya.

Katika Katekisimo Kubwa, Luther husema, "Kila Mkristo ana mambo ya kutosha kusoma na kujizoeza katika maisha yake yote. Daima ana ya kutosha kutenda ili aamini kwa uthabiti yale ambayo Ubatizo huahidi na kuleta – ushindi dhidi ya mauti na Ibilisi, msamaha

wa dhambi, neema ya Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu pamoja na vipawa Vyake." Na "Kwa hiyo, ukiishi katika toba unaenda katika Ubatizo, ambao hautangazi tu maisha haya mapya, bali pia huyafanyiza, huyaanzisha na kuyakuza." Katika Ubatizo, tunapatiwa neema, Roho na nguvu za kumshinda mtu wa kale, ili mtu mpya aweze kuibuka na kuinuka na kukua imara. Kwa hiyo, Ubatizo, hubaki milele . . . Kwa hiyo, toba si lolote isipokuwa kuurudia na kuujongelea Ubatizo."

## Kwa Nini Watoto Wachanga Wanabatizwa?

Watoto wachanga wanabatizwa kwa sababu zile zile zinazowafanya watu wazima wabatizwe – kwa sababu ya amri na ahadi ya Mungu. Kile kinachoahidiwa katika Ubatizo kinapatiwa wote wanaokipokea. Kwa hiyo, watoto wachanga pia wana ahadi ya Mungu. Wao pia, wanafanywa wana wa Mungu. Wao pia, wanajumuishwa katika maneno, "mataifa yote" (Mat. 28:19). Yesu huwaalika watoto hasa waje Kwake (Luka 18:15-17). Lakini muhimu ni, kama wenye dhambi, watoto wachanga wanahitaji kile ambacho Ubatizo hukitoa.

Kwa Neno Lake, Mungu aliumba vyote vinavyoonekana na visivyoonekana. Kwa Neno Lake, Bwana wetu Kristo aliita maiti kutoka kaburini (Yohana 11: 43-44). Kitoto ambacho hakijazaliwa, Yohana Mbatizaji, kikaruka tumboni mwa mamake kilipolisikia Neno la Mungu (Luka 1:41-44). Kwa nini shaka lolote liwepo kwamba, katika na kwa njia ya Neno na ahadi ya Ubatizo, Mungu hutoa kipawa kile kile cha imani katika mtoto mchanga? Tukifahamu Ubatizo vibaya kuwa kazi yetu, basi, daima tutautilia shaka. Tunapotambua kwamba, [Ubatizo] si kazi yetu, bali ahadi na kazi yenye rehema ya Mungu, tutatambua kwamba, watoto wachanga wanapaswa kubatizwa na kupokea hazina zitolewazo katika na kwa njia ya Ubatizo.

Sikitiko ni kwamba, kuna watu binafsi na makundi ya makanisa yanayokataza Ubatizo kwa watoto wachanga. Hawaamini kwamba watoto hawa wanahitaji kile kinachotolewa na Ubatizo Mtakatifu. Hawaamini yale Biblia hufundisha waziwazi, yaani, kwamba, Mungu hutuokoa kwa njia ya Ubatizo. Matokeo ya mafundisho haya ya uongo ni kwamba, wanajinyima wenyewe na wanawanyima wengine nguvu, baraka na faraja ya Ubatizo Mtakatifu. Huo ni msiba, maana ni kosa baya sana dhidi ya Mungu kukataza kile ambacho amekitangaza waziwazi katika Neno Lake: "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu" (Matendo ya Mitume 2:39) na "Ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi" (1 Petro 3:21).

## Mwisho

"Tunaona Ubatizo ulivyo tendo kubwa na bora sana, ambalo hutupokonya kutoka kwa kinywa cha Ibilisi na humfanya Mungu kuwa wetu wenyewe, hushinda na kusafisha dhambi na humwimarisha mtu mpya kila siku. [Ubatizo] hubaki daima mpaka tutakapotoka katika msiba wa sasa na kuingia katika utukufu wa milele" (Katekisimo Kubwa).

Maana, nguvu na ahadi ya Ubatizo Mtakatifu huwa hasa juu ya Yeye aliyeishi bila kosa kwa ajili yetu na ambaye aliteseka na kufa kama fidia ya kuchinjwa kwa dhambi za ulimwengu. Alifufuka akashinda mauti na kaburi. Katika Ubatizo Mtakatifu, tunapokea baraka zote za dhabihu ya Kristo ya kupatanisha. Mshukuruni Mungu kwa kipawa Chake cha Ubatizo Mtakatifu!

Daktari A. L. Barry<br>
Rais<br>
Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri